



# MRADI WA BILIONI 17.89 WASAINIWA

■ Utanufaisha zaidi ya Wakazi 400,000 **uk 2**



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa CCECC, Zhang Junle wakitia saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji Sahwa.

**MRADI WA MAJITAKA  
MWANZA UNAVYOVUTIA  
WAGENI DUNIANI**

**uk 7**

**UJENZI MRADI WA  
MAJI MAGU WAFIKIA  
ASILIMIA 85**

**uk 3**



Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imetiliana saini na Mkandarasi Kampuni ya China Civil Engineering Construction Cooperation (CCECC) ya China kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Butimba hadi Igoma.

Tukio hili la kihistoria lime-shuhudiwa Aprili 16, 2019 katika Kata ya Lwanimah wilayani Nyamagana na wakazi wa Jiji la Mwanza ambao walipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali katika kuwahakikisha huduma ya majisafi na salama inawafikia wananchi wote.

Akizungumza wakati wa tukio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga aliseme ujenzi wa mradi ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji ya Uganda wa Ziwa Victoria na kwamba fedha za ujenzi wake zimetolewa na Serikali ya Tanzania.

"Mradi huu utagharimu jumla ya Shilingi Bilioni 17.89 ambazo zimetolewa na Serikali ya Tanzania kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD)," alisema Mhandisi Sanga.

Kwa mujibu wa Mhandisi Sanga ni kwamba mradi unahuishwa ulazaji wa Bomba kuu la kusafirisha maji kutoka katika chanzo kipy cha Butimba hadi Tenki la Igoma kupitia eneo la Sahwa, ujenzi wa Kituo cha Kusukuma maji Sahwa, ujenzi wa tenki la chini ya ardhi la kuhifadhi maji lenye ukubwa wa kuhifadhi lita milioni 2 za maji katika eneo la Sahwa.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana Dkt. Philis Nyimbi akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela alimtaka mkan-darasi wa mradi kuhakikisha anatekeleza mradi kama ilivyo kwenye mkataba ikiwa ni pamoja na kuzingatia ubora na muda wa ujenzi.

Dkt. Nyimbi alisisitiza umuhimu wa ubunifu kipindi chote cha utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha mradi unaleta tija iliyokusudiwa.

Mradi huu unatekelezwa kwa Miezi 24 kuanzia Aprili, 16 siku ambayo Mkataba ulisainiwa rasmi.

Kukamilika kwa mradi huu kutowezesha upatikanaji wa huduma ya maji kwa Wakazi wapatao 400,000 wa Jiji la Mwanza hususan wa maeneo ya Uganda wa Kusini mwa Jiji hasa ikizingatiwa kwamba utanufaisha maeneo ya Wilaya tatu ambazo ni Nyamagana, Illemela na Misungwi.

# MRADI WA BILIONI 17.89 WASAINIWA



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa CCECC, Zhang Junle wakitia saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji Sahwa.

# UJENZI MRADI WA MAJI MAGU WAFIKIA ASILIMIA 85

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira

(MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga amesema ujenzi wa mradi wa majikatika Mji wa Magu, Mkoani Mwanza umefikia asilimia 85 za ujenzi wake.

Mhandisi Sanga alisema hayo alipofanya ziara kwenye mradi huo Aprili 24 kwa lengo la kujionea na kujiridhi-sha hatua iliyofikiwa ya ujenzi wake ambao unasimamiwa na MWAUWASA kwa niaba ya Wizara ya Maji.

Mhandisi Sanga alisema ute-kelezaji wa jumla wa mradi umefikia asilimia 85 na ulazaji wa bomba kwa ajili ya kuunganisha wananchi imefikia asilimia 95.

Alibainisha kwamba mradi una uwezo wa kuzalisha lita 7,250,000 am-bayo ni mahitaji ya Mji wa Magu kwa miaka 20 ijayo. "Mradi huu ni mkubwa sana hata kama wananchi wa Magu wataongezeka mara mbili zaidi bado ut-aweza kuwashudumia," alisema Mhandisi Sanga.



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) akielekeza jambo wakati wa ziara yake ya ukaguzi wa ujenzi wa mradi wa maji Mji wa Magu Katikati ni mwakilishi wa Mhandisi Mshauri, Mhandisi Adam Jabir.



Muonekano wa Mji wa Magu kutoka kwenye usawa lilipo tenki la kuhifadhi maji la mradi.

Mhandisi Sanga alisema kuka-milika kwa miradi inayotekelzeza chini ya ufadhili wa Serikali kuitia mpango wa Uboreshaji wa Huduma ya Majisafi na Usafi wa

Mazingira Ziwa Victoria, miji yote mikuu ya Mkoa wa Mwanza itakua imepata huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria.

"Mradi ukikamilika miji yote mikuu ya Mkoa wa Mwanza itakua imepata huduma ya maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria kwani tumepeleka Nansio, Sengerema, Ngudu, Magu na Misungwi," alisema.

Mhandisi Sanga aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Mwanza na wa Wilaya ya Magu kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwenye shughuli mbalimbali za utekelezaji wa mradi.

Aidha, aliwapongeza wananchi kwa ushirikiano wanaoutoa hususan wa ulinzi wa miundombinu ya maji inayotumika kwenye ujenzi wa mradi huo.

**Bodi ya  
Uhariri**

**Mohamed Saif**  
Assistant  
Manager Public  
Relations  
MWAUWASA

**Ikupa Enock**  
Graphic Designer



**LIMETOLEWA NA:**  
Mamlaka ya Majisafi  
na Usafi wa Mazingira  
Jijini Mwanza  
(MWAUWASA).



*East Africa  
City at optimal cost*

**0800110023**

**mwauwasatz**

**mwauwasa**



Mkuu wa Wilaya ya Magu Mkoani Mwanza, Dkt Philemon Sengati ameipongeza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa usimamizi mahiri wa mradi wa maji unaotekelozwa wilayani humo.

Pongezi hizo amezitoa jana wilayani humo wakati wa ziara ya ukaguzi wa hatua ya utekelezaji wa mradi wa maji ili kujiridhisha na utekelezwaji wa mradi.

Katika ziara hiyo, Dkt. Sengati aliambatana na Msimamizi wa ujenzi wa mradi kwa niaba ya Wizara ya Maji ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga aliyeongozana na wataalam wengine.

Dkt. Sengati alisema ameridhishwa na namna ambavyo MWAUWASA chini ya kiongozi wake Mhandisi Sanga inavyosimamia ujenzi wa mradi huo.

"MWAUWASA inafanya kazi nzuri sana, binafsi nimeridhishwa na utekelezaji wa huu mradi na namna ambavyo MWAUWASA inausimamia," alisema Dkt. Sengati.

Akizingumzia utekelezaji wa mradi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga alisema mradi wa maji Magu unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali kwa asilimia 100 na utekelezaji wa jumla wa mradi umefikia asilimia 85 na ulazaji wa bomba kwa ajili ya kuunganisha

wananchi imefikia asilimia 95.

Mhandisi Sanga alisema mradi wa maji Magu ni mkubwa ikitilinganishwa na miradi mingine ya Misungwi na Lamadi ambayo kwa pamoja inatekelezwa kuititia Mpango wa Uboreshaji wa Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Ziwa Victoria (LV WATSAN).

Alisema mradi una uwezo wa kuzalisha lita 7,250,000 ambayo ni mahitaji ya Magu kwa miaka 20 ijayo. "Mradi huu ni mkubwa sana hata kama wananchi wa Magu wataongezeka mara mbili zaidi bado utaweza kuwashudumia," alisema Mhandisi Sanga.

Aliongeza kuwa kukamilika kwa miradi inayotekelozwa chini ya ufadhili wa Serikali kuititia mpango wa LV WATSAN, miji yote mikuu ya Mkoa wa Mwanza itakuwa imepata huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria.

"Mradi ukikamilika miji yote mikuu ya Mkoa wa Mwanza itakuwa imepata huduma ya maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria kwani tumepeleka Nansio, Sengrema, Ngudu, Magu na Misungwi," alisema.

Mhandisi Sanga aliupongeza uongozi wa Mkoa wa Mwanza na wa Wilaya ya Magu kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa kwenye shughuli mbalimbali za utekelezaji wa mradi.

Aidha, aliwapongeza wananchi kwa ushirikiano wanaoutoa hususan wa ulinzi wa miundombinu ya maji inayotumika kwenye ujenzi wa mradi huo.

"Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhe. John Mongella na Mkuu wa Wilaya ya Magu, Dkt. Sengati kwa uhamasishaji walioufanya kwa wananchi kuchangamkia mradi ikiwa ni pamoja na kuachia njia ya kulaza mabomba kwani yanapita kwenye maeneo yao," alisema.

Naye mwakilishi wa Mhandisi Mshauri, Mhandisi Adam Jaber alielezea hatua iliyofikiwa ya ujenzi wa mradi na alisema kwamba Tenki Linalojengwa lina uwezo wa kuhifadhi lita milioni 2 za maji na hatua iliyopo ya ulazaji wa mabomba kwa wananchi imefikia kilomita 65.

# DC MAGU AIPONGEZA MWAUWASA



Wananchi waliokusanyika kumsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Magu, Dkt Philemon Sengati wakati wa ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa mradi kwenye maeneo ya makazi.





# WANANCHI

## 12,000 NYASHIMO WILAYANI BUSEGA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA

Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) imesaini mkataba na Mkandarasi Kampuni ya BENNET Contractors Ltd ya Mkoani Mwanza kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa maji wa Nyashimo, Wilayani Busega Mkoani Simiyu utakaonufaisha wananchi wapatao 12,000 wa vitongoji vya Bukabile, Bulima na Mwagulanga.

Hafla ya utiaji saini ilifanyikia Mei 10, 2019 Wilayani Busega na kushuhudiwa na wananchi, watendaji wa Serikali na viongozi mbalimbali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Anthony Mtaka ambaye alibainisha kwamba zaidi ya asilimia 74 ya

wananchi wa Busega watakuwa na uhakika wa maji safi na salama mara baada ya kukamilika kwa mradi.

Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga akiieleza utekelezaji wa mradi huo alibainisha kuwa ni maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli baada ya ahadi aliyoitoa kwa wananchi wa Nyashimo ya kuwapelekea maji safi na salama.

"Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli alivyopita hapa Nyashimo wakati wa ziara zake aliwaahidi wananchi wa hapa kuwatatulia kero ya maji na aliagiza Wizara ya Maji kuhakikisha inatekeleza mradi haraka iwezekanavyo," alisema Mhandisi Sanga.

Mhandisi Sanga alisema mradi utatekelezwa kwa Miezi 15 na utagharimu jumla ya Shilingi Bilioni 1.8 na kwamba unafadhiliwa kwa asilimia 100 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania.

Kwa upande wake Mhe Mtaka alisitisitza mradi ukamilike kabla ya muda uliopangwa wa miezi 15 na alimtaka Mkandarasi kuhakikisha analifanya kazi suala hilo na alisema endapo kama Mkandarasi atabaini urasimu katika utekelezaji wa mradi amfahamishe haraka ili kuondoa hali hiyo.

"Tumeambiwa mradi unate-



kelezwa kwa miezi 15, lakini tunahitaji ukamilike kabla ya hapo, tunahitaji ukamilike haraka iwezekanavyo, Mkandarasi kama unaona kuna maeneo kuna urasimu nifahamishe hapa hapa," alisitisitza Mtaka.

Aliongeza kuwa utekelezwaji wa mradi ni neema kwa wananchi wa Busega na aliwasihhi kuchangamkia fursa zitokanazo na ujenzi wake kuanzia hatua za awali za utekelezaji na alimuagiza Mkandarasi kuhakikisha anatekeleza mradi kwa ufanisi mkubwa na kutoa kipaumbele kwa jamii inayozunguka kuwa ya kwanza kunufaika.

Alisema Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli inatoa kipaumbele kwa Wakanadarasi wazawa na alimtaka Mkandarasi wa mradi kutomuangusha Mhe. Rais.

"Mheshimiwa Rais anajitahidi kuwajengea uwezo wakandarasi wa ndani sasa na nyie msimvunje moyo, fanyeni kazi vizuri aendelee kuwaamini ili mfanye na mradi mingine 05 m i k u b w a .

Mkandarasi unapofanya vizuri unajiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata kazi zingine", alisema.

Aliongeza kuwa mbali na manufaa yatakayopatikana baada ya ujenzi kukamilika, zipo fursa zingine ambazo zinapatikana wakati wa ujenzi ambazo alisitisitza zinapaswa kunufaisha jamii inayozunguka mradi kwanza ili kujenga uhusiano imara na hivyo kurahisisha utekelezaji wa mradi.

"Mradi unapaswa kujibu mahitaji ya jamii, unaleta neema nyingi ikiwemo ajira na fursa zingine za kibiashara nitarajia manunuvi ya ndani yataanzia hapa ikiwemo saruji na hata kutumia magari ya mchanga ya hapa," alisitisitza.

Mtaka alimpongeza Mhandisi Sanga kwa jitihada zake na umahiri wa kusimamia miradi anayokabidhiwa kwa niaba ya Wizara ya Maji na alimsitisitza aendelee na moyo huo wa kizalendo na aliipongeza Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi wa MWAUWASA.

Inaendelea uk 6

# **WANANCHI 12,000 NYASHIMO WILAYANI BUSEGA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA**

## **Inatoka uk 5**

"Mhandisi Sanga hakuna asiyekufahamu kwa utendaji wako wa kazi, hii miradi unayoismamia itakupa baraka kwa Mungu. Tungependa uwe sehemu ya mafanikio ya Mkoa wetu wa Simiyu," alisema.

Naye Mbunge wa Jimbo la Busega Mkoani Simiyu, Dkt. Raphael Chegeni ambaye alikuwa mionganini mwa viongozi walioshuhudia tukio hilo alisema kero kubwa waliyokuwa nayo wananchi wa jimbo lake ni ukosefu wa maji safi na salama na tayari mwarobaini wake umepatikana.

Dkt. Chegeni alipongeza jitiha-

da za Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli katika kutimiza ahadi alizotoa kwa wananchi wakiwemo wa jimbo lake na alibainisha kuwa utekelezaji wa miradi ni maelekezo ya Rais na kwamba kwa Wilaya ya Busega ipo miradi mingi inatekelezwa na aliitaja baadhi ambayo ni ya Kiloleli na Lamadi. "Mheshimiwa Rais anafanya kazi kubwa ya kututatulia matatizo yetu, hapa tatizo kubwa lilikuwa ni maji. Rais wetu mpendwa ametimiza ahadi yake ninamuunga mkono kwa asilimia mia moja," alisema.

Vilevile alipongeza jithada za Mkuu wa Mkoa wa Simiyu na MWAUWASA kwenye utekelezaji wa miradi na aliwaasa wananchi kushiriki ipasavyo kwenye ujenzi wa mradi sambamba na kulinda na kutunza miundombinu yake kwani ni wajibu wa kila mwananchi kufanya hivyo kwa manufaa yake na ya vizazi vijavyo. Kwa upande wake, Mwakilishi wa Mkandarasi, Sabato Boas alihidi kutekeleza mradi kwa muda mfupi kadri itavyowezekana na kwa utaalam un-aotakiwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa kwenye mkataba.





Ugeni kutoka Brazili, Afrika Kusini, Kenya na Uganda ukiwa katika moja ya eneo lenye mradi wa majitaka wa simplified sewerage Jijini Mwanza.

# MRADI WA MAJITAKA MWANZA UNAVYOVUTIA WAGENI DUNIANI

UPATIKANAJI wa majisafi na salama katika Jiji la Mwanza ni miongoni mwa mambo yanayopewa umuhimu mkubwa kwa sasa.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), inaendelea na juhudzi zake za kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji ikiwemo maeneo ya pembezoni.

Juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa na MWAUWASA kuhakikisha wananchi wote wanafikiwa na huduma ya maji kama ambavyo Serikali ya Awamu ya Tano ilivyoelekeza.

Mbali na usambazaji wa miundombinu ya majisafi na salama, lakini MWAUWASA pia inatekeleza ujenzi wa mradi wa mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka kwenye maeneo ya milimani unaofahamika kitaalamu kama "Simplified Sewerage System";

Hivi karibuni mamlaka ilipokea ugeni kutoka asasi za kiraia kutoka Brazil, Afrika Kusini,

Kenya na Uganda. Nchi hizo zimevutiwa na ubunifu uliotumika katika ujenzi wa mradi huo wa uondoshaji majitaka kwenye maeneo ya milimani.

Katika mahojiano maalumu na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya kijamii nchini (CCI), Dk. Tim Ndezi, anazungumza mambo mbalimbali kuhusu ugeni huo.

Dk. Ndezi ndiye alikuwa mwenyeji wa ugeni huo kwa hapa nchini, anasema mradi huo umeendelea kuwa kivutio kikubwa kwa mataifa mbalimbali duniani.

Anasema taasisi zinazojishughulisha na masuala ya usafi wa mazingira kutoka nchi mbalimbali ulimwenguni baada ya

kupata sifa za mradi huo zimevutika kujifunza zaidi ubunifu uliotumika katika utekelezaji wake ili pia kuutumia katika nchi wanazotoka.

"Wageni hawa wamekuja kujifunza namna ambavyo mradi huu umejengwa ili nao wakaandae mradi wa namna hii kwenye nchi zao," anasema Dk. Ndezi.

Mradi huu umeendelea kutembelewa na wageni kutoka mataifa mbalimbali kwa lengo la kujifunza namna uliyotekeliza na namna ambavyo unaendeshwa.

Kwa mujibu wa Dk. Ndezi, ugeni huo ulilenga kuzungumza na wanufaika wa mradi huo ili kufahamu wajibu wao na namna ambavyo waliupokea na njia wanazotumia kuutunza.

Hii ni mara ya pili kwa mwaka huu, mradi huo kutembelewa na ugeni kutoka nje ya nchi, ambapo hivi karibuni MWAUWASA ilipokea ugeni kutoka Kenya ambao walifika kwa ajili ya kujifunza namna bora ya kutekeleza mradi wa majitaka hususan kwa maeneo yasiyo rasmi.

Ugeni huo wa awali kutoka nchini Kenya ulieleza namna uliyoyutiwa na ubunifu mkubwa uliotumika katika ujenzi wa mradi wa majitaka kwenye maeneo ya milimani.

Wageni hao kutoka Kenya walihidi kurejea tena nchini na wataalamu wa mamlaka zinazohusika ili kujenga miradi ya namna hiyo nchini kwao.

### UGANDA WAZUNGUMZA

Mmoja ya wageni kutoka Uganda, Mundamba Omar, anasema nchi hiyo inayo changamoto ya wananchi wake hususan wa kipato cha chini kuskosa mfumo bora na rasmi wa uondoaji wa majitaka.

# MRADI WA MAJITAKA MWANZA UNAVYOVUTIA WAGENI DUNIANI



## Inatoka uk 7

Anasema ziara hiyo waliyofanya Jijini Mwanza imewapatia uzoefu na ujuzi wa namna ya kujenga na kusimamia mradi mzuri wa majitaka. "Tunaipongeza MWAUWASA, kazi iliyo fanyika hapa ni ya kipekee, hatuna budi nasi kuiga," anasema Omar.

Ikumbukwe kwamba mradi huo ulikuwa mionganoni mwa miradi miwili bora zaidi kutekelezwa Barani Afrika, chini ya ufadili wa African Infrastructure Trust Fund (EU-AITF).

### MHANDISI SANGA

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga, ujenzi wa mradi ulianza mwaka 2016 na umenafaisha kaya zipatazo 415.

Mhandisi Sanga anasema mradi wa Simplified Sewerage ulijengwa kwa majoribio kwenye maeneo matatu ambayo ni Kilimahewa, Mabatini na Igogo.

Katika maeneo hayo, Mhandisi Sanga anasema mwitikio ulikua mzuri na alitolea mfano kwa Kilimahewa ambapo MWAUWASA ilipanga kuunganisha kaya 68.

Hata hivyo, kutokana na mwitikio kuwa mkubwa, kaya 117 ziliunganishwa na kwa upande wa Mabatini mpango ulikua ni kuunganisha kaya 88, ambapo zaidi ya kaya 178 ziliunganishwa na kufikia jumla ya kaya 415 kwenye maeneo yote matatu.

Mhandisi Sanga anabainisha kuwa awamu ya pili ya ujenzi wa mradi, itahusisha maeneo mengi zaidi ambayo ni Kabuhoro, Ibungilo, Kawekamo na Isamilo.

"Maeneo ambayo tulianza nayo kwenye awamu ya kwanza nayo hatujamaliza, kwa hiyo haya ni maeneo mapya, lakini pia tutarudi kwenye hayo maeneo ya awali tukaunganishe kaya zilizosalia," anabainisha Mhandisi Sanga.

Akielezea sababu za mradi huo kuitwa simplified, Mhandisi Sanga anasema mradi ulipunguza baadhi ya vigezo kwenye miongozo ya usanifu miradi kutocha Wizara ya Maji.

"Ukivifufuta vigezo vyote kama vilivyo kwenye miongozo inakua ngumu kutekeleza mradi kwenye maeneo ya namna hiyo," anasema.

Anaongeza changamoto iliyopo kwenye Jiji la Mwanza ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya maeneo hususan ya milimani hayajapimwa, hivyo kusababisha ujenzi wa miradi kuwa mgumu.

Anabainisha kwa Tanzania, Jiji la Mwanza ni la kwanza kutekeleza miradi ya namna hiyo na kwamba kwa duniani miradi ya namna hiyo inapatikana nchini Brazili.

Mhandisi Sanga anasema lengo

mahsus la mradi ni kuondosha majitaka kwa njia rahisi kutoka kwenye maeneo ya milimani ili kuwaepusha wakazi na maradhi yanayoweza kutokea kutohana na mfumo usio rasmi wa uondoshaji wake.

"Lazima tuhakikishe majitaka yanatolewa na yanatibiwa kwa kuwa haya yanaweza kuwa ni hatari kwani mara nyingine hua ni chanzo kikuu cha maradhi," anasema.

Anasema awali uondoshaji wa majitaka kwenye maeneo ya milimani Jijini Mwanza ulionekana kuwa mgumu na kutowezekana. "Ni lazima tuwe na majawabu kwenye maeneo ambayo hapo zamani ilionekana hayawezekani kabisa," anasema Mhandisi Sanga.

### DIWANI

Diwani wa Kata ya Mbugani, Athumanji Jama, anasema kabla ya mradi huo hali ilikuwa ni chafu hasa ikizingatiwa hali halisi ya kijigrafia ya maeneo ya milimani. "Walikuwa wakichimba yooo vifupi na wakati wa mvua hali inakuwa tete sana, maji yalikuwa yanatiririka oyo na magonjwa ya mlipuko yalikuwa ya kufikia tu," anasema Jama.

Baadhi ya wananchi wanaiomba MWAUWASA kuharakisha ujenzi wa mradi mpya ili kaya nyingi zaidi zinufaikie.



# MWAUWASA 'TUNAJADILI NA KUTEKELEZA'

Kama ilivyo ada, Wafanyakazi wa MWAUWASA hukutana kila mwezi mara moja kupitia mukutano wa Mkurugenzi na Wafanyakazi wa kila mwanzo wa mwezi ili kujadili masuala mbalimbali ya kiutendaji kwa lengo la kuhakikisha mwana-nchi wa Jiji la Mwanza anapata huduma bora.

Mukutano huo huju muisha wafanyakazi wote wa MWAUWASA ambapo taarifa mbalimbali za kiutendaji hu-jadiiliwa sambamba na kutafuta ufumbuzi wa pamoja wa changamoto za kiutendaji ambazo huwasilishwa na wafanyakazi kwa njia ya majadiliano. Aidha, mukutano huo pia hutumika kuwaponeza wafanyakazi wanaokuwa wamefanya

vizuri kwa kutazama Kanda ambayo inakua imepata alama za juu za kiutendaji katika mwezi husika kupitia Mfumo wa Upimaji wa Utendaji wa watumishi Kikanda ambao uliana rasmi kutumika hapo Agosti, 2018 baada ya kuzinduliwa rasmi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Profesa Kitila Mkumbo.

Mfumo huo hutumika kuwapima watumishi kiutendaji kwa kutumia vigezo vitano ambavyo ni mauzo, makusanyo, maunganisho mapya ya wateja, uharaka wa kuttatu malalamiko ya wateja hususan suala zima la upatikanaji wa maji na udhibiti wa upotevu wa maji kwa kiwango kinachokubalika.

Kwa Mwezi Aprili, 2019 Kanda iliyoongoza kiutendaji kwa vigezo vilivyoolezwa hapo mwanzo ni Kanda ya Nyegezi ikifuatiwa na Kanda ya Mjini Kati, Makongoro na mwisho ni Kanda ya Nyakato. Hata hivyo kwa Mwezi Machi, 2019 Kanda iliyoongoza ilikuwa ni Nyakato.



Baadhi ya wafanyakazi waliohudhuria mukutano huo na wawakilishi wa Kanda zilizoshinda mara baada ya kupokea zawadi.



Baadhi ya viongozi wa mitaa kutoka Kata ya Nyamhongolo walipokutana na wawakilishi wa MWAUWASA (hawapo pichani) ili kujadili namna bora ya kuwa na mradi endelevu wa maji kwenye maeneo yao.

## MWAUWASA KUENDELEZA USHIRIKIANO NA JAMII

Ushirikiano na Jamii ni nyenzo muhimu am-bayo hutumiwa na Mamlaka ya

Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) katika uendeshaji wa shughuli zake.

Kupitia ushirikiano huo na Jamii, MWAUWASA imefanikiwa kupunguza kero mbalimbali kwenye maeneo inayofikisha huduma kwani changamoto nyingi zinapata ufumbuzi kupitia ushirikiano huo wa pamoja.

“Tunafanya kazi kwa kushirikiana na Jamii, tunajadili kwa pamoja changamoto mbalimbali hususan ya upungufu wa maji kwenye maeneo ya

pembezoni kwa lengo la kupata ufumbuzi wa pamoja,” anasema Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga.

Utaratibu huu wa ushirikiano na Jamii pia unaratibiwa kupitia program ya

‘Zungumza na MWAUWASA’ ambayo ilianzishwa kwa ajili ya kujadiliana na wananchi juu ya kero walizonazo kwenye suala zima la huduma ya maji.

Programu hii ni endelevu na in-aendeshwa kwa mpango wa mikutano am-bayo huitishwa na Wenyeviti wa Mitaa kwa kushirikiana na MWAUWASA.

Faida ya Programu hii ni pamoja na Mwananchi kupata fursa ya kueleza kero kuhusiana na suala zima la huduma ya maji; Kupata utatuzi/ufumbuzi wa pamoja wa kero; Mwananchi kupata elimu ya masuala mbalimbali yanayohusu maji na Mwananchi kupata fursa ya kuelewa shughuli zinazofanywa MWAUWASA.



Hatua ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa tenki la maji Nyamhongolo ilipofikia. Mradi huu unatarajiwa kukamilika kwa wakati.





# ADHA YA MAJI KUWA HISTORIA

**D**hamira ya Serikali ni kuwaondolea adha wananchi kwa kuwafikishia huduma ya majisafi na salama.

Katika kuahakikisha dhamira hiyo inafikiwa, Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli imeendelea kutekeleza

miradi mbalimbali ya maji kwa lengo la kuwasogezza huduma ya majisafi na salama wananchi wake.

Hivi karibuni maeneo ya Kanda ya Ziwa Victoria yalishuhudiwa matukio matatu makubwa ya kihistoria kwenye Mikoa ya Mwanza na Simiyu ya utajii saini wa miradi mikubwa ya maji.

Utajii saini huo kwa nyakati tofauti ulishuhudiwa na mamia ya wananchi wa maeneo husika amba walipongeza jithada za Serikali za kuwaondoshea adha walivodumu nayo kwa kipindi kirefu.

### SAHWA, NYAMAGANA- MWANZA

Serikali kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) ilitiliana saini na Mkandarasi Kampuni ya China Civil

Engineering Construction Cooperation (CCECC) ya China kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Butimba hadi Igoma utakaonufaisha wananchi wapatao 400,000 wa maeneo ya Ukanda wa Kusini wa Jiji la Mwanza.

Tukio hili la kihistoria lilishuhudiwa Aprili 16, 2019 katika Kata ya Lwanima Wilayani Nyamagana na wakazi wa Jiji la Mwanza amba walipongeza jithada zinazofanywa na Serikali katika kuwahakikisha huduma ya majisafi na salama inawafikia wananchi wote.

Ujenzi wa mradi huo ni sehemu ya utekelezaji wa Programu ya Uboreshaji wa huduma ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Miji ya Ukanda wa Ziwa Victoria na utagharimu kiasi cha Shilingi Bilioni 17.89 am-bazo zimetolewa na Serikali ya Tanzania.



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (Kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya HALEM, Mhandisi Happy Lebe wakikabidhi ana mkataba wa utekelezaji wa mradi wa maji Nyampande. Wanaoshuhudia ni viongozi wa Mkoa wa Mwanza.



Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) na Mwakilishi wa Kampuni ya BENNET Contractors Ltd, Sabato Boaz (kulia) wakisaini mkataba wa ujenzi wa Mradi wa Maji wa Nyashimo-Busega, Mkoani Simyu. Wanaoshuhudia ni viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Simiyu na Wilaya ya Busega.



Mkurugenzi Mtendaji MWAUWASA, Mhandisi Anthony Sanga (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya CCECC wakisaini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji wa Sahwa.

### NYAMPANDE, SENGEREMA- MWANZA

Mei 09, 2019 tukio la kihistoria lilishuhudiwa huko katika kijiji cha Nyampande Wilayani Sengerema la kuwahakikisha wananchi wa maeneo hayo wanaondokana na adha ya muda mrefu ya upatikanaji wa maji.

Serikali kupitia MWAUWASA ilitiliana saini ya ujenzi mradi wa maji wa

Bilioni 1.8 na Mkandarasi Kampuni ya HALEM ya Jijini Dar es Salaam mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa wakazi wa Kata ya Nyampande, Wilaya Sengerema Mkoani Mwanza ya kuwaondolea adha ya upatikanaji wa maji.

Mradi huu, utanuafisha vijiji vya Nyasenga, Kawekamo na Nyampande vyenye jumla ya wakazi wapatao 16,000 amba wata-pata huduma ya majisafi.

unasimamiwa

na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA) kwa niaba ya Wizara ya Maji.

Ni historia adhim kwa wananchi kushuhudia tukio la utajii saini wa mikataba ya ujenzi wa miradi mikubwa ya maji ambayo ilikuwa ni kilio chao cha muda mrefu na hatimaye Serikali imesikia na ufumbuzi umepatikana.

Viongozi mbalimbali walishuhudia matukio hayo ya kihistoria na walipata fursa ya kutoa maelekezo ya utekelezaji wake ambapo waliwataka wakandarasi wanaojenga miradi kuwahakikisha wanaikamilisha kwa wakati na kwa ubora na vigezo vinavyokubalika. Tunatekeleza kwa vitendo, Hakuna Atakayeachwa.

### NYASHIMO, BUSEGA- SIMIYU

Mei 10, 2019 wananchi wa Mji wa Nyashimo (Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Busega) walipata fursa ya kushuhudia utajii saini mkataba wa ujenzi wa mradi wa maji Nyashimo utakaonufaisha wananchi 12,000 kutoka vitongoji vitatu vya Bukabile, Bulima na Mwagulanja.

Utajii saini huo ulikuwa baina ya MWAUWASA (Msimamizi wa Mradi) na Mkandarasi kampuni ya BENNET Contractors Ltd ya Mkoani Mwanza kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji wa Nyashimo utakaoghami kiasi cha Bil 1.8.

Ujenzi wa miradi ya maji ya Nyashimo

# WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA AWEKA JIWE LA MSINGI MRADI WA MAJI MJI WA MISUNGWI

**MRADI WA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA WA ZIWA VICTORIA KATIKA MJI WA MISUNGWI MKOANI MWANZA**

*Jina la Mradi – Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Ziwa Victoria katika mji wa Misungwi.*

*Eneo Mradi ulipo – Kijiji cha Nyahiti na Mjini Misungwi katika Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi Mkoani Mwanza.*

**Mmiliki – Wizara ya Maji**

**Thamani ya Mradi Tsh Bilioni 12.85**

**Mfadili wa Mradi – Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

*Lengo la Mradi – Kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama kwa wakazi wa sasa wa Nyahiti na Misungwi na uwezo wa mradi ni kuhudumia zaidi ya wananchi 64,000.*



Waziri Mkkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa (kulia) wakimsikiliza, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga (kushoto) alipotoa maelezo kuhusu ujenzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mji wa Misungwi katika kijiji cha Nyahiti Mkoani Mwanza, Machi 19, 2019. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkkuu)



Waziri Mkkuu, Kassim Majaliwa akikagua ujenzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mji wa Misungwi katika kijiji cha Nyahiti Mkoani Mwanza, Machi 19, 2019. Kushoto kwake ni Waziri wa Maji, Profesa, Makame Mbarawa na kulia kwake ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkkuu)



Waziri Mkkuu, Kassim Majaliwa akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mwanza (MWAUWASA), Mhandisi Anthony Sanga kuhusu michoro ya Mradi wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira wa Mji wa Misungwi kabla ya kuweka jiwe la msingi la Mradi huo, Machi 19, 2019. Wa pili kulia ni Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa, kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella na wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Juma Sweda. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkkuu)



Waziri Mkkuu, Kassim Majaliwa akipongezwa na Waziri wa Maji, Profesa Makame Mbarawa baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mji wa Misungwi katika kijiji cha Nyahiti Mkoani Mwanza, Machi 19, 2019. Kulia ni Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Mwanza, Anthony Daallo. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkkuu)



Waziri Mkkuu, Kassim Majaliwa akikagua mashine za za kusukuma maji kabla ya kuweka jiwe la msingi la Mradi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa Mji wa Misungwi katika kijiji cha Nyahiti Mkoani Mwanza, Machi 19, 2019. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkkuu)

# SALAM ZA MKURUGENZI

*Ndugu Mda,*

Tunakupongeza sana kwa ushirikiano unaoendelea kutupa ikiwemo taarifa unazotupatia kuhusiana na huduma tunayotoa. Nakufahamisha kwamba taarifa hizi tunazopata kutoka kwako zimekuwa na msaa-da mkubwa sana kwetu katika suala zima la utoaji wa huduma.

Tunakuomba kwa heshima na taadhima usichoke kutupatia ushirikiano kila inapobidi, utukumbushe pale tunapojisahau, utusahi-hishe pale tunapokosea.

Tunapenda kukufahamisha kwamba kupitia ushirikiano wako, tumeweza kupunguza kero mbalimbali zilizokuwepo hapo awali kwenye mitaa mbalimbali tunayoihudumia.

Ikitoea kutoridhishwa na huduma kwa namna yoyote ile, tafadhalii usisite kutufahamisha, tupo hapa kwa lengo kuu la kukupatia huduma inayostahili. Aidha, tunaomba taarifa za mivujo na taarifa zingine pia unaweza kutupigia kupitia namba 0800110023 (Bure) na ukatupa taarifa hizo.

Kumbuka kwamba namba hizo za simu ni za Kitengo chetu cha Huduma kwa Mteja na hautolipia gharama za mawasiliano kwani gharama zote zinabebwa na MWAUWASA.

Aidha, napenda kukufahamisha kwamba tunatambua yapo maeneo ambayo bado yanachangamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji, hatupo kimya jitihada za dhati tunaendelea nazo kuhakikisha tunakabiliana na changamoto hiyo. Ndugu mdau, ipo miradi mingi tunayoendelea nayo, ni imani yangu kwamba mara baada ya kukamilika kwake huduma itaimarika maradufu. Tunomba uendelee kutuvumilia na tuendeleze ushirikiano wetu kwani kwa pamoja tutafika mbali. Tushirikiane kulijenga Jiji letu la Mwanza.

*Mhandisi Anthony Sanga  
Mkurugenzi Mtendaji  
MWAUWASA*



# MIKUTANO NA WADAU



Kutoka kulia waliokaa ni Kaimu Mkurugenzi MWAUWASA, Meck Manyama, Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Salum Kalli, Mjumbe wa NEC, Jamal Babu na Katibu wa Vijana CCM Mkoa wa Mwanza, Luhende. Waliosimama nyuma ni watendaji kutoka CCM na MWAUWASA

Lengo letu ni kuhakikisha huduma inaimarika kwenye maeneo yote. Na ili kuhakikisha lengo hili linatimia, tunaendeleza utamaduni wetu wa kukutana na wadau mbalimbali na kujadili namna bora ya kuboresha huduma.

Hivi karibuni tulikutana na

Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mwanza ili kujadili masuala mbalimbali ya kuboresha huduma zetu sambamba na kuimarisha uhusiano.

Mingoni mwa masuala yaliyojadiliwa ni Mkakati wa kuhakikisha huduma inaimarika hu-

susan kwa wananchi wa maeneo ya pembezoni, uharaka wa kuwafikia wananchi kunapotokea hitilafu ama mkwamo wa huduma, taarifa kwa wateja kunapotokea mabadi-liko ama pale ambapo huduma itakuwa haipatikani.